ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe

32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Arobaini – Tarehe 10 Agosti, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Fatma Mbarouk Said (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kuhusu ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

KAULI ZA SERIKALI:

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kunijaalia kuwa na afya njema na sote hapa Mwenyezi Mungu atuzidishie umrii mrefu na siha njema ili tuweze kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa ufanisi.

Mhe. Spika, aidha nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kunipa fursa ya kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011. Mhe. Spika, kwa namna ya pekee napenda nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein kwa kudhihirisha ninayoyasema kwa siku zisizozidi tatu baada ya kupokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameniagiza ripoti hii sasa niiwasilishe kwenye Kikao cha Baraza la Wawakilishi. Hii inamaanisha kwamba Rais wetu ni muumini nambari moja wa utawala bora basa kwenye misingi ya uwazi na uwajibikaji (*transparency and accountability*).

Mhe. Spika, vile vile napenda kwa mara nyengine tena kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kukubali kuipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2009/2010.

Aidha, vile vile napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* ndugu yangu Omar Ali Shehe Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chake Chake na Wajumbe wake wote kwa umahiri na umakini mkubwa wanaofanya katika kuzifanyia kazi ripoti zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na mashirikiano makubwa wanayotupa katika kutekeleza majukumu yetu.

Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua mahesabu ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yakiwemu Mawizara, Mashirika na Taasisi mbali mbali pamoja na miradi ya maendeleo na kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hiyo inaelezea hali halisi ya mapato na matumizi ya fedha katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nakuonesha udhaifu au dosari na kasoro zozote katika uwekaji wa mahesabu pamoja na kasoro katika udhibiti wa utumiaji wa fedha na mali za serikali.

Madhumuni ni kupata ufanisi katika utunzaji na uendeshaji wa shughuli za serikali na kuhakikisha kwamba sheria na taratibu zote za matumizi na udhibiti wa fedha na mali za serikali zinafuatwa ipasavyo, na kufanikisha lengo kuu la serikali la kuwa na utawala bora unaoheshimu sheria na taratibu zilizowekwa.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984 kifungu 112 (3) cha Katiba ya Zanzibar Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kufanya yafuatayo:-

a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa na iwapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha ziliomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo.

c) Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi hesabu za Mahkama zote za Zanzibar na hesabu za Tume au vyombo vyengine vinavyohusika.

Mkakati wa Kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

Mhe. Spika, ofisi inaendelea kuliwekea kipaumbele suala la mafunzo kwa wafanyakazi kwa kuhakikisha inawasomesha wafanyakazi wake mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika vyuo mbali mbali nchini na nje ya nchi na hasa katika fani mpya za ukaguzi zikiwemo ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa mazingira na ukaguzi wa kompyuta.

Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, ofisi imetumia muongozo wa ukaguzi kwa kufanikisha ukaguzi wa mahesabu ambao unakwenda sambamba na miongozo ya ukaguzi inayokubalika na jumuiya za ukaguzi duniani.

Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeendelea kutoa huduma zake za ukaguzi wa mahesabu kwa taasisi za serikali yakiwemo mashirika mbali mbali pamoja na mahesabu ya Halmashauri za wilaya katika mikoa Unguja na Pemba, pamoja na miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo mbali mbali pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, ofisi imeendelea kukagua mafaili ya mafao ya wastaafu katika kipindi cha Julai, 2010/2011. Jumla ya majalada 1,130 ya wastaafu yamekaguliwa, kati ya hayo 353 yamekaguliwa kwa ajili ya mafao yanayolipwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na majadala 777 ya wastaafu yamekaguliwa kwa ajili ya mafao yanayolipwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*).

Tathmini ya Utekelezaji wa Ripoti iliyopita ya mwaka 2009/2010:

Mhe. Spika, Serikali kupitia taasisi zake kwa kiasi imejaribu kufuatilia hoja na mapendekezo tuliyoyatoa katika ripoti ya mwaka 2009/2010, lakini bado kuna haja kubwa ya kuongezwa juhudi za ufuatiliaji na uajibikaji ili kupunguza au kuondoa kabisa mapungufu ya kihesabu na kiutendaji yaliyobainika katika kipindi hicho.

Uwasilishaji wa mahesabu.

Tathmini iliyofanywa na ofisi imebaini kuna mafanikio makubwa ya uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati kwa kasma za mawizara na taasisi zinazojitegemea.

Mhe. Spika, kwa upande wa mashirika ya serikali bado kuna tatizo kubwa la kutowasilishwa kabisa au kwa wakati mahesabu ya mwisho wa mwaka ambapo ni kinyume na sheria za fedha. Aidha hali hii inapelekea mashirika mengi kutojulikana mwenendo wao mzima wa utendaji. Baadhi ya mashirika hayo ni Shirika la Bima, Mfuko wa Hifadhia ya Jamii, Benki ya Watu wa Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA)*, Shirika la Huduma za Maktaba, Shirika la Umeme, Shirika la Utalii, Shirika la *ZSTC* na Shirika la Meli na Uwakala.

Utunzaji wa Vifaa na Samani za Serikali:

Mhe. Spika, kuhusu udhibiti na utunzaji wa vifaa na thamani za serikali ukaguzi umebaini bado kuna matatizo makubwa katika masuala mazima ya kuzitambua mali hizo, kuzitunza pamoja na kuziwekea kumbukumbu, hali ambayo hupelekea kuwepo uwezekano mkubwa wa kupotea mali hizo bila ya kutambulika.

Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Mwaka 2010/2011

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetoa aina mbili za ripoti zinazohusiana na ripoti ya ukaguzi wa hesabu kwa mawizara. Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi iliyokaguliwa kwa taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ripoti hizo zimekusanya taarifa za ukaguzi wa mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwemo taasisi mbali mbali, mashirika pamoja na miradi mbali mbali ya maendeleo. Ripoti hizi zinajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wahisani wa maendeleo kwa kuzingatia sheria na taratibu ziliopo. Vile vile ripoti zimezingatia matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo pamoja na mapato yaliyokusanywa kutoka vianzio mbali mbali vya mapato ya kawaida na maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, aidha kwa upande wa ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ripoti imekusanya taarifa ya ukaguzi wa mahesabu pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo iliyokaguliwa ikiwemo miradi ya barabara, maji safi na salama, miradi ya afya, miradi ya elimu, miradi ya ujenzi wa miradi mengineyo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ripoti inajumuisha taarifa ya ukaguzi wa miradi hiyo iliyokaguliwa ambapo taarifa ya utekelezaji wake itaelezea hali ya udhibiti na ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Kiwango cha Uwekaji wa Hesabu za Serikali:

Mhe. Spika, kiwango cha uwekaji wa hesabu za serikali kimeimarika kwa kiasi kikubwa hali iliyopelekea wizara na taasisi zake kuweza kufunga na kuwasilisha hesabu zao kwa wakati uliowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha.

Mhe. Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kutoa ushauri na miongozo kwa taasisi mbali mbali za serikali juu ya kuimarisha viwango vya uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu ikiwemo madaftari mbali mbali ya hesabu pamoja na uhifadhi na udhibiti wa vifaa na mali za serikali.

Mhe. Spika, Ofisi inashauri viongozi na watendaji wakuu wa serikali kuwa karibu na watendaji wao katika kufuatilia mwenendo mzima wa fedha kuanzia ukusanyaji wa mapato na matumizi pamoja na uhifadhi na udhibiti wa rasilimali za umma katika taasisi wanazozisimamia, pamoja na kusimamia utekelezaji wa sheria ziliopo. Hali hiyo itaongeza ufanisi, uwajibikaji na utawama bora katika udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha na mali za umma.

Mambo yaliyobainika katika ukaguzi kwa mwaka 2010/2011:

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 hali ya uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu katika taasisi mbali mbali za serikali umeimarika. Hata hivyo, kumejitokeza baadhi ya dosari kiutendaji ambapo hoja mbali mbali za ukaguzi zilizotolewa kuhusiana na dosari hizo ziligundulika. Baadhi ya hoja hizo zilipatiwa ufumbuzi kwa kurekebishwa na kutolewa ufafanuzi pamoja na maelezo yaliyokosekana wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuna udhaifu na matatizo katika masuala ya ufungaji na uwasilishwaji wa mahesabu katika mashirika, kuwepo kwa malimbikizo ya madeni wanayodai au kudaiwa baadhi ya taasisi za serikali. Kuwepo matumizi yasiofuata taratibu za manunuzi kwa mujibu wa sheria ziliopo, kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu katika ukusanyaji wa

mapato, kutokufuatwa makubaliano ya mikataba pamoja na kutokuwepo kumbukumbu za baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa na baadhi ya taasisi za serikali.

Aidha, kumegundulika kujitokeza udanganyifu katika utayarishaji wa mafao ya baadhi ya wastaafu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa upande wa ukaguzi wa mafao ya wastaafu wa Kikosi cha KMKM, kumegundulika kuwepo kwa baadhi ya wafanyakazi waliokuwa wameshastaafu lakini mishahara yao bado ilikuwa inapelekwa kwenye kikosi hicho.

Mhe. Spika, ukaguzi yakinifu uliofanywa kupitia miradi mbali mbali ya serikali ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara, miundombinu ya maji safi na salama, vituo vya fya, ujenzi wa madarasa na huduma mbali mbali za elimu pamoja na miradi ya ujenzi wa ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ukaguzi umebaini miradi mingi haikuweza kufikia lengo lililokusudiwa kulingana na fedha zilizoingizwa na kutumika. Aidha, baadhi ya miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi za serikali haikuweza kukamilika kabisa. Hali hii inasababisha hasara kubwa kwa serikali kwa vile fedha nyingi zimetumika kugharamia miradi hiyo ambapo malengo na tija havikupatikana.

Ukusanyaji wa Mapato ya Kawaida:

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 ukusanyaji wa mapato haukuweza kufikia lengo la ukusanyaji kwani jumla ya shilingi 219 bilioni zilikusanywa, ukilinganisha na makadirio ya shilingi 239.7 bilioni kwa mwaka huu. Ukaguzi umebaini bado kuna fursa nzuri ya kukusanya mapato zaidi iwapo jitihada za makusudi zitachukuliwa katika kuimarisha vianzio mbali mbali vya mapato ya ndani hasa katika sekta ya utalii.

Matumizi ya Kazi za Kawaida:

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 hali ya mgawanyo wa fedha za matumizi ya kawaida yameonesha kuwepo kwa mafanikio makubwa. Ukaguzi uliofanyika umebaini matumizi ya kawaida kwa mwaka 2010/2011 yalifikia asilimia 96.7 ya makadirio.

Matumizi ya Maendeleo:

Kwa mwaka 2010/2011, serikali ilijipangia kutumia kiasi cha shilingi 39.4 bilioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, ambapo jumla ya shilingi 30.4 bilioni zimeingizwa na kutumika kwa kazi mbali mbali za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 77.3 ya makadirio. Aidha, kwa upande wa washirika wa maendeleo serikali ilijipangia kutumia jumla ya shilingi 211.8 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo ambapo jumla ya shilingi 136.27 bilioni zimeingizwa na kutumika ambapo ni sawa na wastani wa asilimia 64.3 ya makadirio.

Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*)

Mhe. Spika, ofisi inashirikiana na kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ripoti yake. Kamati hii ni miongoni mwa kamati muhimu za Baraza la Wawakilishi katika kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma. Tunatoa shukurani za dhati kwa mwenyekiti wa kamati hii pamoja na wajumbe wake kwa mashirikiano mazuri wanayotoa katika kufanikisha majukumu yetu ya kikatiba, kamati imekuwa ikishirikiana na watendaji wa ofisi hii wakati wote wa ufuatiliaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Changamoto:

Mhe. Spika, kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara katika mifumo ya fedha pamoja na viwango vya uwekaji wa kumbukumbu za hesabu na ufungani wa mahesabu ya mwisho wa mwaka, kunasababisha athari katika utendaji wa shughuli za uhasibu na ukaguzi. Tunashauri kuwepo kwa utaratibu wa mafunzo endelevu kwa wahasibu na wakaguzi ili kukabiliana na mabadiliko hayo na kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya viwango vya kitaifa na kimataifa vya uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu pamoja na ufungaji wake.

Mhe. Spika, ukaguzi yakinifu ni ukaguzi ambao unahitaji upatikanaji wa taarifa kamili za fedha na utekelezaji ili kuweza kupima uwiano kati ya matumizi na tija iliyopatikana. Lakini taasisi nyingi zinazotekeleza miradi hiyo zinakuwa hazitoi mashirikiano kwa wakaguzi kuweza kupata taarifa sahihi za miradi hiyo ikiwemo mikataba na makubaliano ya miradi. Fedha zitakazotumika katika mradi huo utaratibu wa uingizwaji fedha na usimamizi wake pamoja na uwajibikaji.

Kutokana na hilo, inakuwa vigumu kuweza kupata taarifa muhimu ambazo zitatoa sura na hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo kama imeweza kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kupima ufanisi katika utekelezaji wake kama hali ya uchumi ilizingatiwa kabla ya kuanza miradi hiyo.

Malengo ya baadae ya Ofisi:

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali tayari imeshatayarisha mpango mkakati (*strategic plan*) mpya ya miaka mitatu kuanzia 2011 – 2014. Mpango wa mkakati huo umejikita katika maeneo ya kuimarisha ofisi kiutendaji pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye taaluma mbali mbali zitakazosaidia kuimarisha kazi za ukaguzi. Mpango wa mkakati huo umekusudia kuendeleza jitihada zilizochukuliwa wakati wa kutekeleza mpango mkakati uliopita wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2007 – 2011, ambapo utekelezaji wake umeleta mafanikio makubwa ya kiutendaji katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Katika mpango mkakati huo, Ofisi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
2. Kushajihisha usimamizi, uwazi na uwajibikaji wa masuala ya fedha na mali za umma na
3. Kushirikiana na kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa taasisi zinazosimamia uwajibikaji pamoja na kuimarisha mawasiliano na wadau wetu.

SHUKRANI:

Mhe. Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada mbali mbali zilizochukuliwa katika kuimarisha ofisi hii kiutendaji na watendaji kwa ujumla. Aidha, nawapongeza wale wote waliochangia kwa njia moja au nyengine hadi kufanikisha kukamilisha kwa ripoti hii, wakiwemo watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa jitihada zao wanazochukua hadi kufanikisha kukamilisha kwa ripoti hii kwa wakati.

Vile vile nawashukuru viongozi na watendaji wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhasibu Mkuu wa Serikali na watendaji wa taasisi mbali mbali za serikali kwa mashirikiano mazuri wanayotupa wakati wa kutekeleza kazi zetu za ukaguzi.

Mhe. Spika, shukurani za dhati kwa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi na wengineo kwa ujumla wao wamechangia maendeleo makubwa yaliyopatikana katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

HITIMISHO:

Mhe. Spika, ili tuweze kufikia malengo ya kupunguza umasikini na kupambana na rushwa, hatuna budi sote tuelekeze nguvu zetu katika kupambana na yale yote yanayosababisha kuendelea na umasikini pamoja na kupambana na vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali za serikali. Aidha, tutahakikisha kwamba sheria nambari 11 ya mwaka 2003 na sheria nyengine zote zinazohusu udhibiti na utunzaji wa fedha na mali za umma zinafuatwa ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora tunakushukuru kwa kuwasilisha ripoti hizo mbili. Taratibu zinatutaka kwamba ripoti hii isijadiliwe kama ilivyo chini ya kanuni ya 43 ya Kanuni zetu za Baraza, lakini kama kuna maswali na hii sio lazima, kama kuna jambo bado halijaeleweka kwenye ripoti hii basi maswali yanaweza kuulizwa na Waheshimiwa Wajumbe. Lakini kwanza nimkaribishe Mhe. Omar Ali Shehe, Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* ili atoe maoni ya Kamati hiyo halafu baadae twende kwa Wajumbe kama kuna maswali. Mwenyekiti wa *PAC* karibu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC)*: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nisome maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika **(***PAC***)** kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika (*CAG*) kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujaalia uhai na afya iliyotufanya tuweze kuendelea kuhudhuria kikao hiki. Aidha, naomba nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa nia ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibibi Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar juu ya uwasilishaji wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2010/2011 katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa namna anavyosimamia vyema majukumu ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, nimpongeze kwa namna alivyowasilisha ripoti za mdhibiti muda mfupi uliopita.

Vile vile niwapongeze watendaji wake kwa kukagua mahesabu, kutayarisha ripoti na hatimaye kuwasilisha katika Baraza hili ambalo ndilo chombo cha wananchi. Ripoti mbili kwa pamoja za mwaka 2010/2011 zinahusu ukaguzi yakinifu pamoja na ukaguzi wa mahesabu kwa mwaka huu.

Mhe. Spika, kwa kuwasilisha kwa ripoti za ukaguzi za mwaka 2010/2011 kunafanya kazi Ofisi ya *CAG* kufanya kazi zake za ukaguzi kuendana na wakati kwa vile kwa sasa taasisi za umma zinajiandaa kufunga na kuwasilisha kwa Mdhibiti mahesabu ya mwaka 2011/2012 kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya fedha kifungu cha 24.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya *PAC* ninatoa pongezi kwa serikali wa namna inavyomuwezesha Mdhibiti na hivyo akaweza kutekeleza majukumu yake na kufanya ukaguzi, kutayarisha ripoti za ukaguzi na hatimaye akaweza kuwasilisha katika Baraza hili.

Aidha kwa niaba ya kamati tunatoa pongezi kwa *CAG* kwa kuweza licha ya changamoto nyingi zinakabili ofisi yake, kuanzisha aina mpya ya ukaguzi yakinifu na akaweza kuendeleza kwa mwaka wa pili sasa, yaani kuanzia 2009 – 2010.

Ni imani ya kamati kuwa changamoto zinazoikabili afisi pamoja na utendaji wa afisi kama vile vilivyoelezwa kwa undani na umakini wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wakati wakichangia hotuba ya Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Afisi yenyewe wizara na serikali zitafanyiwa kazi kwa madhumuni ya kuimarisha utendaji wa afisi hii muhimu kwa taifa kwa maslahi ya wananchi ambao ndio walipa kodi.

Mhe. Spika, uwasilishaji wa ripoti mbili hizi za 2010/2011 ambazo zimegusa ukaguzi katika wizara 14, taasisi 21, mashirika ya umma 6, mikoa 5, Manispaa na Halmashauri za Mabaraza ya Mji 6 na vikosi 5.

Miradi 12 kwa wizara nane unafanya Baraza letu sasa kuwa ripoti na ripoti 5; 3 za 2009/2010 na 2 za 2010/2011 ambazo hadi sasa haziguswa kufanyiwa kazi na Kamati yetu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali. Kitendo hiki cha kuwa na ripoti 5 ni changamoto kubwa kwa Baraza letu kwani huenda likapelekea kuwa na mrundikano wa ripoti na hivyo kuachwa nyuma na kasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Mhe. Spika, ili kamati iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi ni muhimu sana kwa Baraza kutenga muda wa kutosha wa kufanya kazi kwa kuzifuatilia ripoti za *CAG*. Ni ukweli ulio dhahiri kwamba kufanya kazi hizi kwa mgao wa wiki mbili mbili tu hautoweza hata kidogo kutufikisha katika lengo tunalokusudia. Tunaamini na ndivyo ilivyo kuwa ili ripoti za ukaguzi ziwe maana ni vyema sana zifanyiwe kazi kwa wakati unaostahiki.

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo yaliomo kwenye ripoti hizi za mkaguzi ambayo kamati yetu inatakiwa kufuatilia na yale yanayohusiana na miradi ya ujenzi, mambo mengine yanayohusiana na manunuzi ya madawa ya kutibu binadamu na wanyama, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na fani nyengine za kitaaalamu, kwani

kamati inaomba Baraza kutenga fungu maalum kwa ajili ya kukodia wataalamu wa fani hizo ili waweze kuisaidia kamati katika kazi zake badala ya kuwa na mtaalamu wa fani ya mkaguzi pekee.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo kamati yetu imekuwa ikilisikitikia sana ni suala la utekelezaji wa maoni ya kamati hii mara tu yanapowasilishwa Barazani na kupelekwa serikalini pamoja na suala la kuipatia kamati mafunzo maalum yahusianayo na ukaguzi yakinifu kama vile kompyuta na mazingira.

Mhe. Spika, ni vyema tukakumbuka kwamba kazi ya ukaguzi ina gharama kubwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatumia fedha nyingi kuifanya kazi hii na hatimaye ripoti hiyo inapofanyiwa kazi na Kamati ya *PAC* japo kuna gharama nyengine ni busara mno kuthamini nguvu za gharama hizo za walipa kodi wa nchi hii ili tunusuru upotevu wa fedha kizembe. Vyenginevyo tusipotilia maanani maoni hayo basi ni dhahiri tunaongeza hasara isiyo na sababu na inayoepukika.

Mhe. Spika, nisingependa hata kidogo kusahau nguvu na michango mikubwa yenye busara ya Wajumbe wa Kamati ya *PAC* ambao kwa kweli utendaji wao wa kwenye kamati usiojali muda na hali, umeniwezesha mimi binafsi kufanya kazi hii ya uenyekiti kwa kujiamini mno nikiamini jeshi langu lililonizunguka.

Mhe. Spika, itabidi kwanza niombe samahani niweze kukirudia tena kifungu hiki.

Nisingependa hata kidogo kusahau nguvu na michango mikubwa yenye busara ya Wajumbe wa Kamati ya *PAC* ambao kwa kweli utendaji wao kwenye kamati usiojali muda na hali, umemuwezesha binafsi mwenyekiti wetu kwa kujiamini mno kwa kuamini jeshi lililozunguka.

Mhe. Spika, naomba niwatambue kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Omar Ali Shehe	Mwenyekiti
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Mjumbe
4. Mhe. Farida Amour Mohamed	Mjumbe
5. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Mjumbe
6. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Mjumbe
7. Mhe. Shamshi Vuai Nahodha	Mjumbe
8. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad	Mjumbe
9. Ndg. Othman Ali Haji	Katibu
10.Ndg. Amour Mohamed Amour	Katibu

Mhe. Spika, mwisho naomba nichukue nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Katibu wa Baraza kwa usikivu wake na msaada na mashirikiano yake kwa kamati na bila ya kuwasahau Makatibu wetu wa kamati ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kuratibu shughuli zetu ambazo zimeiwezesha kamati kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Spika, niwashukuru Wajumbe wenzangu wote wa Baraza kwa utulivu na uvumilivu wao kwa muda wote ambao nimekuwa nikitoa hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Makamo Mwenyekiti tunakushuru kwa ripoti hiyo uliyoitoa kwa niaba ya kamati. Basi tuende kwenye maswali, turuhusu maswali kiasi ambapo nimemuona Mhe. Salmin Awadhi Salmin aliyetangulia baadae Mhe. Hija Hassan Hija na baadae Mhe. Ali Abdalla Ali.

Mhe. Salmin Awadhi Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili tu. Lakini kabla ya hayo niwapongeze kamati hii inayosimamia suala hili la udhibiti wa pesa za serikali PAC, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kwa kweli Mhe. Spika, inaonekana bado wapo nyuma kutokana muda basi tuwaombee waongezewe muda ili waweze kufanya kazi zao vizuri Muda unaonekana hautoshi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Mhe. Waziri mwaka jana au kwenye ripoti yake ya mwisho ambayo aliwasilisha hapa, Waheshimiwa Wajumbe walieleza concern yao juu ya hatua mbali mbali zinazochukuliwa juu ya kasoro hizi ambazo zinajitokeza mara kwa mara, ambapo kila ripoti inapokuja basi makoseo yanakuwa yanajirudia rudia, jambo ambalo inaonekana kwamba hakuna hatua zinazochukuliwa.

Sasa Mhe. Waziri ukatuahidi kwamba utachukua hatua, sasa ninataka utueleze Mhe. Waziri ni hatua gani ambazo umezichukua tokea taarifa ile ya mwisho iliyokuwa imewasilishwa kwako, matatizo yaliyojitokeza hadi kufikia taarifa hii. Hilo moja.

Lakini la pili ripoti hii imeonesha kuna baadhi ya taasisi kushindwa kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na inasema kwamba kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria, sheria iliyopitishwa na Baraza lako tukufu.

Tunavyofahamu sisi kwamba mtu anapokwenda kinyume na sheria kunakuwa na adhabu, sasa atwambie wale wote ambao wamekwenda kinyume na sheria hii au sheria za serikali zilizopitishwa na Baraza hili, ni hatua gani ambazo zimechukuliwa juu ya wale watu ambao wamekwenda kinyume na sheria ambazo zimepitishwa hapa au atueleze kwamba sheria hiyo iliyopitishwa hapa haikuweka adhabu.

Lakini jengine la tatu la mwisho Mhe. Spika, kuna baadhi ya taasisi za serikali zimekusanya mapato makubwa, lakini makusanyo hayo hayakuingizwa katika hesabu za kikosi za mwisho wa mwaka kwamba wamekusanya mapato. Sasa pia atueleze na hili nalo kwenda kinyume na masuala ya fedha. Ni hatua gani za kisheria zitachukuliwa dhidi ya taasisi hizi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi ninaomba kukushukuru na ninaomba nimuulize Mhe. Waziri maswali yangu yafuatayo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema katika ripoti yake kwamba kumejitokeza udanganyifu wa baadhi ya wafanyakazi wakati wa kutoa mishahara na viinua mgongo na ametoa mfano wa Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu. Lakini ninaomba kumuuliza inakuwaje kutokezea udanganyifu huo wakati kabla ya kutolewa viinua mgongo hivyo, lazima vipitie katika Afisi ya CIG na kuthibitishwa. Hebu atwambie inakuwaje watu kupata fursa hiyo ya kugawana fedha za umma wakati afisi yake ndio yenye mamlaka ya kuthibitisha malipo haya.

Lakini pili Mhe. Spika, Mhe. Waziri amezungumza malengo ya baadae ya afisi yake lakini kadri dunia inavyokua na afisi yake inavyojipanga kunahitajika kuwepo na sheria yenye meno ili kuwawezesha wao kufanya kazi vizuri na kujitegemea kujitawala. Jee, Mhe. Waziri haoni busara sasa afisi yake kuandaa sheria madhubuti itakayowawezesha wetu hawa CIG kuwa na meno katika kufanyakazi zao.

Tatu Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 4 wa ripoti yake aliyoisoma, amesema kwamba wamefanya tathmini ya utekelezaji wa ripoti ya 2009/2010 na wamagundua baadhi ya mambo. Ninavyofikia mimi kwamba ripoti hii haijaenda PAC na ndio maana wakawa na ripoti 5. Sasa atwambie ripoti hii tathmini hii walifanya wapi wakati PAC hawajafanya uchunguzi au serikali hivi sasa imeamua kujichunguza wenyewe.

Nne Mhe. Spika, kutokana na ujanja wa wataalamu wa afisi mbali mbali, kamati yako inapokwenda kufanya uchunguzi PAC na kamati nyengine za kisekta kumekuwa na dosari kubwa…

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe rekebisha hiyo simu kwa bahati mbaya umekuwa ni wewe unayezungumza ingebidi nikukatisha mazungumzo ili utoke nje lakini tuuchukulie ni bahati mbaya, endelea lakini rekebisha hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa busara yako.

Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba kamati zinapokwenda kufanya kazi mbali ya kuwepo Makatibu wa Baraza, lakini kunahitajika kuwepo na maafisa bajeti kutoka Wizara ya Fedha, na zipo taarifa kwamba maafisa hawa wapo tayari kufuatana na kamati zako ili kusaidia ugunduzi wa utekelezaji wa bajeti kwenye wizara mbali mbali.

Jee, Mhe. Waziri kwa sababu yeye afisi yako ni ya utawala bora, haoni kwamba kuna haja sasa ya kukaa na Baraza la Wawakilishi, mbali ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Maafisa wa Baraza la Wawakilishi lakini

tukaambatana na maafisa wa Wizara ya Fedha wanaotoka kwenye Kitengo cha Bajeti ili tukagundua huu ubadhirifu wa pesa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa sababu ya utendaji mzuri wa Kamati ya PAC, afisi yake haioni haja kushawishi Baraza la Wawakilishi na serikali kwa ujumla kuongeza muda kwa Kamati ya *PAC* ili kazi hizi zifanywe kwa ufanisi ili kufikia malengo hayo ya utawala bora.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha taarifa yake kwa uzuri na pia niipongeze Kamati ya *PAC* kwa kazi kubwa inayofanya. Mimi nina maswali matatu.

La kwanza lipo kwenye ukurasa wa 36 ambalo imepigwa picha pale ya jengo la Chuo cha Utawala wa Umma. Ripoti imebaini kwamba mkataba uliowekwa kujengwa jengo lile haukufuatwa, pesa zimetumika nyingi kuliko kazi iliyofanywa. Ripoti imesema kwamba hivi sasa tayari hili jengo limesimama kwa mkataba wa awali; yaani Kikosi cha KMKM waliopewa hivi sasa wamefutiwa mkataba na tayari wamepewa kikosi chengine.

Swali, jee hawa waliokuwa wametumia pesa zaidi ya lile lengo lililokusudiwa hatua gani imechukuliwa dhidi yao au kunyang'anywa kufutwa mkataba imekuwa ndio adhabu yenyewe. Nilikuwa naomba jibu.

La pili ukurasa wa 25 imeonesha orodha ya ujenzi wa njia kutoka Mfenesini kwenda Bumbwini na nyumba zilizovunjwa Shehia ya Kama na watu waliolipwa, kwenye kitabu muna watu wanne tu. Lakini kwa kuwa mimi ni jimbo langu na nilishiriki katika malipo, pale walilipwa watu sita, kwa hivyo watu wawili sikuwaona kwenye kitabu.

Sasa ninataka nijue kwamba wamerukwa ama wamekosewa. Mmoja anaitwa Mohamed Ali Abdalla na mwengine anaitwa Masoud Mohamed Azan. Zimevunjwa nyumba na walilipwa lakini kwenye orodha sikuiona.

Halafu la kuongezea hapo hapo kwenye ujenzi huo nyumba nyingi sana zimeathirika na hivi sasa hazikaliki na tayari taasisi inayohusika ilipita kufanya tathmini, lakini hadi leo sasa hivi unafika mwaka wa pili hakuna jibu, naomba kama jibu mheshimiwa analo ama waziri anayehusika amsaidie ili tuweze kupata jibu.

La mwisho Mhe. Spika, imebainika kwamba taarifa hii sehemu nyingi fedha hazikutumika kama ilivyotakiwa. Sasa naomba nimuulize Mhe. Waziri jee hawa waliokuwa wametumia pesa bila ya taratibu, sheria gani inachukuliwa dhidi yao.

Ninakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii nikauliza maswali mawili matatu katika ripoti iliyowasilishwa hapa mbele yetu ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninataka niulize tu kwa sababu nimeangalia katika ukurasa wa 9 wa kitabu hiki inasema kwamba Wizara ya Fedha wamelipa malimbikizo ya umeme lakini ukaguzi baada ya kutembelea wakashindwa kupata uthibitisho wa wale malimbikizo ya hayo madeni.

Sasa Mhe. Spika, mimi swali langu lipo hapa kwamba kuwa kwanza sijaridhika na maelezo haya kwa sababu kama Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali alikuwa anatakiwa anafuatilia kwa kina mpaka aje na jawabu ya kwa nini malipo haya yalifanywa kwa deni lipi, kwa sababu sasa kama wao hiyo ndio kazi yao.

Bahati nzuri kamati yetu ya *PAC* vile vile ilikuwa na ripoti hii imekwenda kufanya ukaguzi. Sasa leo wao wanasema kwamba wameshindwa kupata hizo taarifa. Sasa hii inakuwa maana yake. Kwa hivyo kuna malipo yamefanywa hewa au kuna malipo yamefanywa bila.

Sasa swali langu lipo hapa, jee sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa ripoti hii tunatakiwa tufanye nini, kwa sababu wao wenye kazi ndio wamesema kwamba hawakupata uthibitisho. Sasa hili nilikuwa ninataka aje nipate ufafanuzi.

Lakini la pili kwa bahati mbaya sana kwamba kuna jenereta ambalo lililonunuliwa na Baraza la Wawakilishi na kama kawaida tunavyosema kwamba ni vizuri taasisi ikafanya matumizi yake wenyewe kutokana na ile bajeti yake, lakini hapa inaonesha jenereta limenunuliwa na taasisi nyengine Wizara ya Fedha likaletwa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo mwenye mali mwengine na aliyenunua mwengine. Sasa swali langu lipo hapa.

Hapa nani anayetakiwa kuwajibika kwa sababu hapa tatizo lililojitokeza kwamba kimekiukwa taratibu za manunuzi baada ya ukaguzi. Sasa nani hapa anatakiwa kuwajibika.

Jengine katika ukurasa wa 12 nimeangalia kuna KMKM lakini kwa kuokoa muda, ninataka nizungumze kwa upande wa vikosi vyote kwa sababu haya madai yaliyoandikwa humu katika ukaguzi yanalingana. Yanalingana kwa sababu katika suala zima la vifungu tulivyovipitisha wao wakafanya kinyume na vile tulivyovipitisha, ndio tulivyozungumza uhaulishwaji wa vifungu bila kuona yale malengo yaliyokusudiwa yanafanyika.

Sasa kitu ambacho ninachosikitika kwamba nimeona kwamba kuna fedha ambazo tulizitenga kwa ajili ya kununulia sare, zimetumika kwa safari za ndani. Kwa hivyo matokezeo yake naona maaskari wanakosa sare kwa sababu fedha zile zinatumika kwa matumizi hayo. Sasa hapa jee Mhe. Spika, swali langu lipo hapa baada ya safari hii na baada ya kurekebisha haya, jee kama litatokezea tena suala hili katika bajeti hii ambayo tumeipitisha ni hatua gani za kisheria zitachukuliwa.

Lakini jengine Mhe. Spika, imeonekana katika ukaguzi kwenye vikosi vyetu hivi kuna madeni yetu mengi ambayo yanayodaiwa vikosi vyetu vya SMZ na madeni haya wenzetu Afisi ya Mdhibiti Mkuu wamesema kwamba baada ya ukaguzi wao wameshindwa kuthibitisha wale au yale madeni kutokana na vielelezo.

Mhe. Spika, mimi ninataka nikuthibitishie mimi nikiwa ni mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mheshimiwa madeni haya pamoja na kwamba hawakuyathibitisha yapo kweli, kwa sababu tunapokwenda kwenye kamati makamanda wanatulalamikia ….

Mhe. Spika: Swali uliza**.**

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa, wanatulalamikia makamanda kwamba kutokana na uingizwaji mbaya wa fedha kwamba mara nyingi wanafika pahala kukopa na madeni haya mheshimiwa yapo mengi na sikuyaona kwenye bajeti hii kwamba kuna bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais kwa kulipa madeni ya wafanyabiashara mbali mbali wanaohudumia vikosi vyetu, na inapelekea wakati mwengine vikosi vyetu kukosa huduma kutokana na madeni ambayo wanayodaiwa. Jee, Mhe. Waziri katika bajeti tuliyopitisha sijui kama fedha hizi za kulipa haya madeni umezitenga au vipi na kama hazikutengwa Mhe. Spika, hawa wafanyabiashara waliotoa huduma kwa vikosi vyetu tunawaweka katika fungu gani.

Lakini vile vile hapa nilikuwa na maombi Mhe. Spika, katika fedha ambazo tulizoziokoa katika wizara mbali mbali, fedha hizi tunashukuru zimetimia bilioni karibu kumi na saba ambazo tulizotenga kununulia meli. Mimi ninadhani ni pahala muafaka tukamega sehemu ya fedha hizi tukaweza kulipa madeni wanayodaiwa vikosi vyetu vya SMZ.

Mhe. Spika: Maswali**.**

Mhe. Hamza Hassan Juma: Aah! maswali na ushauri Mhe. Spika. Huo ulikuwa ni ushauri kwamba fedha hizi zitengwe walipwe wale wanaodai vikosi vyetu vyenginevyo tunaweza tukaja tukakosa huduma.

Sasa Mhe. Spika, kwa kumalizia tu kwamba katika hivi vikosi vya SMZ imeonesha katika ripoti hapa kwamba kuna malipo ambayo wamelipwa vikosi hasa KMKM, mfano kama Mafunzo ambavyo hivi mara nyingi vinajenga katika majengo mbali mbali ya serikali.

Lakini wanasema kwamba malipo yale wameshindwa kuyathibitisha, yaani ile namna walivyolipwa na uwekaji wa mahesabu yao. Sasa Mhe. Spika, nilikuwa ninauliza swali.

Jee, hivi vikosi ina maana hawa wakaguzi wao walipokwenda pamoja na Kamati ya PAC waligundua kwamba haya malipo waliyolipwa hawakufanya kazi walilipwa malipo hewa au tatizo lilikuwa katika uwekaji wa zile kumbukumbu.

Sasa mwisho Mhe. Spika, nina ushauri katika hili suala la vikosi. Tumegundua kwamba vikosi vyetu vya SMZ vikiwemo KMKM pamoja na Mafunzo wanajenga majengo mbali mbali ya serikali, lakini inaonesha kuwa wanajenga kama taasisi za serikali tu. Kwa hivyo inaonesha kwamba hakuna utaratibu mzuri.

Sasa ilikuwa ushauri wangu kwa Mhe. Waziri vikosi zile taasisi za ujenzi zikasajiliwa kama construction company ili kuweza kupata kuondoa hoja hizi ambazo zitakazokuja kujitokeza katika ripoti za Kamati za *PAC*. Kwa sababu vikosi vyetu vinajenga taasisi mbali mbali, mimi siamini kama walikuwa wanalipwa malipo hewa, walikuwa wanalipwa malipo sahihi lakini kwa kuwa kulikuwa hakuna utaratibu wa hizi construction company ndio maana ikaonekana katika vitabu.

Mhe. Spika, kutokana na muda mdogo sikuweza kukimaliza kitabu chote hapo nilipopafikia ninaamini ninaweza nikapata ufafanuzi wa kutosha.

Mhe. Spika, ninakushukuru.

Mhe. Spika: Labda nitoe maelekezo. Haikuwa Baraza hivi sasa kwamba twende ndani ya vitabu hivi na majibu atoe Waziri, hapana.

Ripoti imewasilishwa ili Baraza hili ipokee, kamati inayohusika ije ifanye kazi ilete ripoti baadae ijadiliwe. Sasa Waheshimiwa Wajumbe sio kuingia kwenye kitabu tuanze kumuuliza mheshimiwa hapana, kazi hii tunapewa sisi hapa tupokee kamati ije ifanye, tena mwenyekiti yupo wapi leo, yule pale, ndio utaratibu tunao. (Makofi).

Mhe. Mbarouk Mussa Wadi: Ninakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri maswali.

Mimi nina maswali mawili Mhe. Spika. La kwanza Mhe. Waziri alipokuwa anatupa vitabu vile mwaka jana nilimuuliza swali hapa juu ya zile taasisi za muungano ambazo zinakusanya mapato hapa, kama vile Uhamiaji na nyengine. Nani ambaye anazikagua.

Niliuliza ni kwa nini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Zanzibar hazikagui taasisi hizi. Jee, kulikuwa kuna utaratibu gani ambao utafanywa kuhakikisha Mdhibiti naye anakwenda kuzikagua.

Mhe. Waziri alipotujibu alisema kwamba wapo mbioni katika kukaa pamoja na wenzake wale wa Jamhuri ya Muungano kuhakikisha kwamba zile taasisi za muungano ambazo zinafanyia kazi Zanzibar zikaguliwe na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, nilikuwa ninataka kujua tu suala lile sijui limefikia wapi kwamba sasa limeshakubalika au limefikia hatua gani. Hiyo moja.

La pili Mhe. Spika, vile vile ninarejea mwaka jana wakati ambapo tulipozungumza nilimuuliza Mhe. Waziri hapa juu ya kuisaidia Kamati ya PAC kuweza kuongezewa muda na aliahidi Mhe. Waziri kwamba atakaa na uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba wanalifanyia kazi hili na kulipatia ufumbuzi. Nilikuwa ninataka kujua tu wamefikia wapi na hatua gani wamechukua mpaka hivi sasa.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa nimkaribishe tena Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nataka nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya masuala na nakushukuru vile vile kwa kunisaidia kutoa maelekezo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwamba mimi niliwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Utaratibu ni kwamba baada ya Baraza hili kuzipokea ripoti hizi, maana yake tunaipa Ripoti Kamati ya PAC kwenda kufanyia kazi na watakayoyaona Kamati ya PAC ndio ambayo serikali inatakiwa iyachukue kupitia Baraza hili na kwenda kuyarekebisha au kuyafanyia kazi.

Kwa hivyo, nilichokuwa nikikiona kwamba baadhi ya mijadala ya bajeti ilikuwa ikizungumzwa kwenye ripoti hii. Kwa hivyo, naomba ile yote iliyoelekea kwenye mijadala ya kibajeti na miongozi, naomba nisiitolee ufafanuzi nijibu baadhi ya hoja ambazo moja kwa moja zimekwenda katika ripoti.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimshukuru Makamo Mwenyekiti, wa kamati ya PAC, kwa uwasilishaji wake alioufanya kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya PAC na mimi nataka nichukue fursa hii kukuomba rasmi Mhe. Spika, kwa kupitia Baraza lako tukufu kwamba Kamati hii kwa mujibu wa ripoti zilizorundikana, wanahitaji kupata muda wa kufanya kazi, ni vizuri tukawapa fursa ya kuweza kuzifanyia kazi ripoti hizi ili na wao wakienda sambamba na *speed* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, wakati nakuja kuwasilisha ripoti hizi leo ya mwaka 2010/2011, tayari maandalizi ya ripoti ya mwaka 2011/2012 iko katika utaratibu wa maandalizi, na nategemea kwenye kikao cha Aprili, ripoti ya mwaka 2011/2012 iwasilishwe hapa Barazani. Kwa maana hiyo kama Kamati ya PAC hatukuiwezesha basi Baraza litakuwa nyuma. Kwa msingi huo ni kwamba niwaombe sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, watakuwa hawana mashiko katika wanayoyasema, kwa sababu chombo cha kuweza kuwashauri Wajumbe wa Baraza juu ya masuala ya matumizi ya serikali na mali za umma bado chombo hiki kitakuwa hakijapata taarifa sahihi.

Kwa hivyo, nikuombe sana Mhe. Spika, kupitia Baraza lako tukufu tuweze kuiwezesha kamati ya PAC iweze kufanyakazi. *Speed* ya wizara yangu kupitia Ofisi ya *CAG* na *speed* ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya uwajibikaji, tutaendelea kuwasilisha ripoti mpaka tuwe tunakwenda sambamba na mwaka wa bajeti ili tuone kwamba serikali inakwenda kwa mujibu wa utawala wa sheria.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo kutokana na mchango wa Mhe. Makamo Mwenyekiti kwa niaba ya Kamati. Naomba sasa nijibu maswali kwa baadhi ya Waheshimiwa ambao wameuliza. Nianze na Mhe. Salmin Awadh aliuliza ni hatua gani nilizozichukua juu ya ripoti iliyowasilishwa mwaka jana na mabadiliko gani.

Mhe. Spika, tukiangalia vitabu hivi vya mwaka 2010/2011 tutaona kuna tofauti kubwa kati ya ripoti zilizopita na hii ya mwaka huu. Hatua niliyoichukua kama nilivyosema mwaka jana. Niliwasilisha ripoti hii serikalini kwa maana ya Baraza la Mapinduzi na kila Waziri alielewa nini kasoro ziliomo ndani ya ripoti ile. Kwa maana hiyo ndio maana ripoti ya safari hii inasema kwamba kuna mabadiliko kwa kiasi fulani ukilinganisha na ripoti zilizopita. Watu waliokwenda kinyume na sheria wamechukuliwa hatua gani. Ziko taasisi ambazo zinawajibika kisheria kuwachukulia watu hatua.

Wa kwanza ni yule muajiri ambaye pengine kosa lile litakuwa limetokezea, analiripoti kwenye taasisi zinazohusika. Sasa kazi ya wizara yangu kwa kupitia Ofisi ya Mdhibiti ni kuripoti na sio kuchukua hatua. Kwa hivyo, mimi nadhani wanaohusika wamesikia, sasa wale waliohusika nani anaweza kuwachukulia hatua, basi nadhani wanaweza kuchukua hizo hatua, ikiwa itathibiti kuwa hayo makosa wameyafanya.

Mhe. Hija Hassan Hija, anasema kwa nini umetokea udanganyifu na wakati taarifa hizi za malipo ya mafao huwa zinapitiwa na Ofisi ya CAG. Ni kweli kupitia Ofisi ya CAG ndio tumegundua udanganyifu na kwa upande wangu kama Waziri wa Utawala Bora, kwa wale ambao tumedhani wamehusika na kadhia hii, kwanza tumeanza kuwachukulia hatua za nidhamu na tunaendelea na uchunguzi. Tukithibitisha kwamba na wao moja kwa moja wamehusika na kadhia hii, kama tulivyochukua hatua kwenye Wizara ya Miundombinu kwa afisa ambaye na Mhe. Hija Hassan sio kwamba huyu afisa alitoa taarifa za wakubwa ndio akachukuliwa hatua. Siku ile sikupata nafasi ya kukujibu. Lakini afisa huyu anashukiwa kuhusika na matukio mengi ya udanganyifu katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Hata ile kadhia ya uajiri alihusika nayo afisa huyu.

Mhe. Spika, hata hili suala la udanganyifu la kuongeza kiwango cha mshahara kwa mstaafu kinyume na kiwango chake halali cha mshahara alikifanya huyu. Kwa hivyo, hatua ya mwanzo tumemsimamisha kazi, tumetoa agizo kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano asimamishwe kazi na hatua nyengine zinachukuliwa. Kwa wale maafisa wetu waliohusika na kama wapo watakaohusika katika ofisi ya CAG, katika hili hakuna *compromise*, hakuna mkubwa wala mtoto wa mkubwa tutawachukulia hatua.

Jengine alilouliza Mhe. Hija Hassan ni kuhusu maandalizi ya sheria. Nataka nikuarifu rasmi kwamba sheria nambari 3 ya Mdhibiti tayari iko kwa Mwanasheria Mkuu inakamilishwa utaratibu wake, na tunategemea ndani ya kipindi hiki, sidhani kama tutawahi katika kikao cha mwezi wa Oktoba, lakini kwenye kikao cha Januari tunatarajia sheria

ile tuiwasilishe hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi, sheria ile tunaifanyia marekebisho kutokana na mapungufu mengi ambayo tunayaona hivi sasa kiutekelezaji yanatupa shida. Kwa hivyo tuendelee kustahamili sheria hiyo itakuja pengine kwenye kikao cha mwezi wa Januari.

Mhe. Spika, kuna mambo yameripotiwa hapa kwamba je, serikali imeamua kujichunguza yenyewe kabla ripoti haijaja kwa Mdhibiti. Afisi ya Mdhibiti kwa mujibu wa sheria ina wajibu wake ndio hizi ripoti ambazo tumezileta. Sasa leo hii nimezi-*table* hapa Barazani, mmepata fursa Waheshimiwa Wajumbe kuuliza maswali, baadae Baraza litafanya kazi yake ya kuipokea, baada ya kuipokea Kamati ya PAC tutaikabidhi rasmi na wakati huo sasa itakuwa ni kazi na jukumu la Kamati ya PAC kwenda kufanyakazi kwa niaba ya Baraza na hatimaye Kamati ya PAC italeta taarifa zake hapa. Kwa hivyo, tulichofanya sisi tumefanya wajibu wetu na PAC itafanya wajibu wake na hatima Baraza litafanya wajibu wake. Kwa hivyo, sio kwamba tunajichunguza wenyewe tumefanya wajibu wetu.

Mhe. Spika, utaratibu wa maafisa kufuatana na Kamati. Nafikiri huko nyuma kulikuwa na utaratibu huo, kila Kamati inatafuta afisa kutoka kwenye sekta wanafuatana naye ili kusaidia baadhi ya maelezo. Lakini katika suala zima la utawala bora na mgawanyo madaraka. Mimi nadhani sasa hivi Baraza limejijengea uwezo wa kuwa na maafisa mbali mbali na wenye taaluma mbali mbali, ndio maana zamani sisi Kamati tulikuwa tuna Katibu mmoja, sasa hivi tuna makatibu wawili katika kila Kamati. Madhumuni yake maafisa wale au makatibu wale ni kuwasaidia Wajumbe wa Kamati kuweza kupata uelewa katika kufanya shughuli zao. Pia tuna kitengo cha utafiti hapa, kimeanzishwa, kama nilivyomsikia Mhe. Hamza Hassan na Wajumbe wengine wamesema. Madhumuni yake kile kitengo ni kufanya utafiti juu ya zile kazi ambazo zinafanywa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo, pale ambapo serikali inatakiwa kutoa msaada wa maafisa fulani kusaidia Kamati. Mimi nadhani serikali iko tayari kwa hilo hakuna tatizo, nafikiri tutalifanyia kazi. Niipigie debe kamati ya PAC, naendelea kuipigia debe Mhe. Spika, iwezeshwe. Lakini mimi kwa upande wangu kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama nilivyosema mwaka jana kuwa kila fursa ya mafunzo yanapopatikana iwe nje au ndani ya nchi, basi ofisi yangu itafanya kazi hiyo. Kwa kupitia bajeti ya mwaka huu tunayo kasma fulani kwa ajili ya Kamati ya PAC. Kwa hivyo, nataka niwahakikishie kwamba kwa sababu sisi tunategemea kuwa PAC inasaidia sana katika kufanyakazi na katika kufikia malengo ya utawala bora. Hii kwetu tunaona kama ni sehemu ya wadau katika kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Ali Abdalla Ali, aliuliza ni hatua gani kwa kikosi cha KMKM kuhusu masuala ya kazi ya ujenzi wa Tunguu. Hatua nilishaieleza kwenye bajeti yangu kwamba na sina hakika kama siku ile ulikuwa wewe kwenye kiti au la, lakini ulikuwa wewe kwenye kiti. Katika majukuisho yangu nilieleza kwa upana kabisa. Sasa kwa sababu ya utaratibu wa kanuni naomba hilo nisilirejee, uende ukatafute *hansard* utaona nini nilichokisema juu ya hatua ambazo zitachukuliwa. Lakini nataka nikuthibitishie kwamba chuo sasa hivi kiko katika hatua za mwisho katika eneo la chini kukamilika na tunatarajia mwanzoni mwa mwezi wa Septemba wanafunzi watahamia kwenye jengo letu la Chuo cha Tunguu kwa kile kikosi ambacho tumekipa kazi.

Watu waliorukwa inawezekana pengine ni *typing mistake*. Lakini zipo taratibu gani kwa wale wengine ambao nyumba zao ziliorodheshwa kama alivyoelekeza Mhe. Spika, hilo itakuwa ni vizuri zaidi ukilielekeza suala hilo kwa wizara inayohusika, maana mimi hapa itanipa tabu, kwa sababu sina kumbukumbu wala sina taarifa sahihi juu ya suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu taratibu za kisheria kama nilivyosema juu ya wale waliohusika na makosa yale kama nilivyojibu mwanzo.

Mhe. Hamza Hassan Juma, alisema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wafanye nini juu ya ripoti hii. Nimeshaeleza cha kufanya nafikiri Wajumbe wa Baraza hili wanakielewa.

Mhe. Spika, kuhusu ununuzi wa jenereta la Baraza la Wawakilishi. Nalo hili ni jambo ambalo lilikuwa likijadiliwa sana hapa. Lakini mimi nataka nitoe maelezo mafupi tu kuhusu suala hili, pengine labda suala linaweza likaja. Bajeti ya manunuzi ya jenereta ilikuwa Baraza la Wawakilishi au ilikuwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kama bajeti ile haikuwa ndani ya fedha za matumizi ya Baraza la Wawakilishi, maana yake watakaohusika katika kuulizwa swali lile watakuwa ni Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, sio Baraza la Wawakilishi. Kama fedha zile ziliingizwa ndani ya kasma ya Baraza la Wawakilishi, basi watakaostahiki

kuulizwa maswali watakuwa ni Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa uelewa wangu hivyo ndivyo ambavyo naweza kulisema.

Mhe. Spika, kulikuwa na maswali mengine yaliyojitokeza huko. Mfano, makosa yaliyojitokeza kwenye vikosi, kama litatokezea tena ni hatua gani zitachukuliwa. Sio kama litatokezea tena, kwa maana kama litatokezea watu wasamehewe halafu wafanye tena kosa ndio ichukuliwe hatua. Kwa kweli kosa ni kosa haina muda maalum, haina wakati wa mwanzo wala wakati wa pili. Kwa hivyo, kama mtu kafanya makosa atachukuliwa tu hatua za kisheria inapothibitika kwamba amefanya hilo kosa.

Mhe. Spika, nakushukuru mambo mengine umeyatolea maelezo sina haja ya kuyarejea aliyoyazungumza Mhe. Hamza Hassan Juma.

Kuhusu maelezo ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Mwaka jana niliahidi juu ya taasisi za Muungano kukaguliwa na *CAG*. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, jana alilieleza vizuri sana. Kilichokuwa kinatutatiza ni Msimamizi Mkuu wa Wizara ya fedha kule. Bahati nzuri Mkaguzi wa Mahesabu Tanzania Bara bado yuko chini ya wizara ya fedha. Sasa wakati ule kumpata Waziri yule aliyekuwepo ilikuwa kazi kubwa sana, Mhe. Omar Yussuf jana alieleza. Lakini kwa sababu ya usikivu wa waziri ambaye yuko sasa hivi, mimi nadhani tutashirikiana na Waziri mwenzangu wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili kuona kwamba tunawasiliana ili hizi kazi kama kuna uwezekano tunaweza tukaangalia sheria kama kuna uwezekano basi ziweze kufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, lakini jana alitoa ufafanuzi juu ya mahesabu ya *migration*. Alisema pale wizarani pana kitengo, lakini kama ni Mdhibiti na yeye ajiridhishe, nafikiri tunaweza tukaandaa utaratibu mzuri wa kuweza kuona Mdhibiti anafanyaje katika kuzifuatilia hizo hesabu za *migration* pamoja na vyombo vyengine vya taasisi za Muungano.

Kuhusu muda wa PAC. Ni kweli na mimi pia siridhiki na muda huo ambao mnaupata na bado naendelea kuwa mimi ni mpiga debe wenu kwa Mhe. Spika, na serikali kwamba mpewe muda zaidi ili muweze kwenda na wakati. Sio kwamba kwenda na wakati kuwa hamjui mnachokifanya, hapana. Lakini muda ambao mnaupata wa kuzifanyia kazi ripoti ni mdogo. Kwa hivyo, ni lazima tukubaliane kwamba Baraza li-*sacrifice* lijue kwamba lazima Kamati ya PAC kutokana na kazi walizonazo waweze kupewa muda zaidi.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Nawashukuru vile vile wale wote ambao wameniuliza maswali nategemea tutaendelea kushirikiana katika kufanikisha kazi hii ya udhibiti wa sera za serikali na mali za umma.

Kwa mara nyengine tena Mhe. Spika, niruhusu nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein. Sio kawaida kwa Rais kumpelekea ripoti baada ya siku tatu akakuagiza kuiwasilisha kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini Rais huyu Dk. Shein kwanza ni *fast reader*. Ukimpelekea kitu anakisoma na anakupa jibu hana kisisi yaani hana ajizi. Kwa hivyo, namshukuru sana kwa muongozo wake na kwa umahiri wake na kwa uwajibikaji wake katika kuitumikia nchi na wananchi wa Zanzibar kwa jumla. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijasema muipokee hii ripoti, nataka niseme jambo moja niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba huko nyuma tulikuwa na tatizo kubwa sana la kukatika katika kwa umeme humu ndani, na tukaielekeza serikali kwamba iangalie jambo hilo kwa kutafuta jenereta lililokuwa kubwa kwa dharura, ili liwahi hasa kwenye kikao cha bajeti iliyopita.

Nichukue nafasi hii kuishukuru sana serikali, wamefanya kazi hiyo kwa sababu kukatika kwa umeme ilikuwa kunatufanya tufanye matumizi makubwa sana kwa kuakhirisha vikao kwa sababu umeme hakuna. Kuwepo kwa jenereta hilo linatuwezesha hata umeme ukikatika tuendelee na shughuli zetu. Naipongeza serikali kwa kushirikiana na Ofisi hii ya Baraza ili kuendesha shughuli zake kwa ufanisi na hilo lilinunuliwa kwa dharura. Sasa kama kuna matatizo ya *procurement*, tujue hiyo ilikuwa ni dharura. Yaliyotoka maelekezo kwenye chombo hiki. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe, nione kama ripoti hii tunaipokea kwa kuwauliza, wanaoipokea ripoti wanyanyue mikono. Wanaokataa. Ripoti imepokelewa na Baraza na sasa iko tayari kwa Kamati ya PAC kuifanyia kazi na pigo la debe kwamba Kamati ya PAC ipewe muda wa kutosha Spika, amesikia ataelekeza hivyo.

Tunawashukuru Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma kwa mara ya kwanza mswada wa sheria ya marekebisho ya sheria ya usajili wa Mzanzibari Mkaazi nambari 7 ya mwaka 2005 na mambo mengine yanayohusiana na hayo ahsante. Naomba usomwe kwa mara ya kwanza. Ahsante.

Mhe. Spika: Madhumuni ya mswada kusomwa mara ya kwanza na kwa sababu ni jambo jipya kidogo. Madhumuni yake ni kwamba tunatoa taarifa kwa Baraza hili kwamba mkutano ujao kazi moja wapo itakuwa ni kujadili mswada huu wa sheria. Suala kama hili hakuna maelezo yoyote isipokuwa taarifa ni kwa Waheshimiwa Wajumbe na baada ya kuwasilishwa kusomwa kwa mara ya kwanza, maana yake ni kwamba Kamati inayohusika baadae itakwenda kuupitia mswada huo ambao tayari nakala zake tunazo.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mswada wa sheria ya usajili wa taasisi za biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo, naomba usomwe kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, naomba niwasilishe mezani mswada wa sheria ya kuanzishwa kwa wakala wa usajili wa biashara na mali Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo, naomba usomwe kwa mara ya mwanzo.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Mswada umesomwa kwa mara ya kwanza, nakala za mswada huu zipo katika Baraza hili nategemea tayari zimegaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe na itakuwa ni kazi ya Kamati baada ya hapa kuzipitia, halafu mkutano ujao utashughulikia kujadili mswada huu utakapokuja kusomwa kwa mara ya pili. Sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mswada wa sheria ya usajili na usimamizi wa maafisa wa afya ya jamii na mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo, kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba tena kuwasilisha juu ya meza mswada wa sheria kuhusiana na hifadhi na usimamizi wa vihatarishi vya afya ya jamii na afya ya mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo, kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru. Mswada umesomwa kwa mara ya kwanza na tayari basi umewasilishwa nakala zake zipo hapa na Wajumbe nafikiri wanazo, Kamati inayohusika itafanya kazi ili hatimaye uje kusomwa kwa mara ya pili kwa mjadala kwenye kikao kijacho. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa kwa siku ya leo zimekamilika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, naomba nichukue nafasi hii, kuna kazi moja ambayo Baraza hili lilinituma nifanye na nikawa kwa muda wote nilikuwa natafakari, ili hatimaye kabla ya kuondoka kwenye mkutano huu kazi hiyo ambayo Waheshimiwa Wajumbe mulinituma tuifanye rasmi.

Waheshimiwa Wajumbe, mtakumbuka kwamba mnamo tarehe 13/07/2012 wakati wa mjadala wa Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Waheshimiwa Wajumbe walio wengi walielezea tatizo linalohusu migogoro ya ardhi. Kwa hivyo, Wajumbe walio wengi waliona kwa ukubwa wa matatizo ya migogoro ya ardhi ingefaa Baraza liunde Kamati Teule.

Jambo hili lilikubalika kwa Waheshimiwa Wajumbe wote kwa upande wa *backbenchers* na serikali, kwa sababu wakati wa majumuisho Mhe. Waziri moja kwa moja alikubali, kwamba ingefaa Baraza hili limsaidie kwa kuunda Kamati Teule, ili iweze kufuatilia migogoro hii mbali mbali. Kwa hiyo, hakukuwa na hoja rasmi ingawa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alichomeka na madhumuni yake ninayajua kuchomeka ile hoja. *(Makofi)*

Lakini jambo lenyewe tayari limeshakubalika Waheshimiwa Wajumbe wengi walilisema na Mhe. Waziri akasema kwa kweli na mimi naona nisaidiwe, yaani nakubali hiyo Kamati Teule iundwe. Kwa maana hiyo, kulikuwa na *consensus* kwa pande zote mbili kwa upande wa serikali pamoja na Waheshimiwa Wajumbe.

Waheshimiwa Wajumbe, wakati tuko kwenye Kamati ya Matumizi Mhe. Mbarouk Wadi Mussa nilimueleza kwamba jambo hilo tayari limeshakubaliwa rasmi kwa pande zote mbili, yaani upande wa *backbenchers* na ule wa serikali. Kwa hivyo, ile hoja ikawa sasa imeanguka juu ya mwamba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kutokana na *consensus* hiyo iliyotolewa na chombo hichi hapo tarehe 13/07/2012 nimewateua Waheshimiwa Wajumbe wafuatao kuwa ndio Wajumbe wa hiyo Kamati Teule. Wajumbe wenyewe ni:-

1. Mhe. Abdalla Moh'd Ali,
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said,
3. Mhe. Ali Mzee Ali,
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla na
5. Mhe. Nassor Salim Ali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nimejaribu kwa kiasi kikubwa kuepuka kuwateua Wajumbe hao kwa hao kuingia kwenye Kamati Teule, kwa sababu tunaelewa mambo yenyewe yanavyokua. Kwa mfano, inaweza kujitokeza kwamba sasa Spika kuna watu anawapendelea humu ndani, lakini kumbe Waheshimiwa Wajumbe sote tuko sawa, tunao uwezo sawa. Kwa hivyo, wajumbe hao ndio watakaofanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Hadudi za rejea katika *Hansard* iliyopatikana kutokana na michango yenu Waheshimiwa Wajumbe, mlielekeza mambo yafuatayo ndio yafuatiliwe katika migogoro hiyo ya ardhi. Jambo hili halikuwa rahisi kwa sababu mambo haya yako mengi mno na kuna mengine yanaeleweka kwamba yako Mahakamani yanasubiri uamuzi.

Hivyo, tuelewe kwamba mambo yalioko Mahakamani Kamati itakuwa haina nafasi kuweza kuyafuatilia kwa mujibu wa Kanuni zetu mpaka pale chombo cha kutoa haki, yaani Mahakama itakapotoa uamuzi wake.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa maelekezo ambayo niliyatoa na baadhi ya maeneo yapo kwenye *Hansard* na hapa naeleza ile misingi tu, lakini *Hansard* itaelekeza hata maeneo moja moja ambayo Waheshimiwa Wajumbe muliyasema na yote yanahusu migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, hii itakuwa ndio sehemu ya hadudi za rejea ambayo Wajumbe nyinyi mulipendekeza kwamba hiyo Kamati Teule ifuatilie, ili hatimaye ilete ripoti katika Baraza hili. Masuala yenyewe ni kama ifuatavyo:-

Maeneo ambayo yanayomilikiwa kuwa umiliki wake umefutwa kutoka kwa watu waliopewa umiliki wa maeneo hayo bila ya taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria. Sasa hayo maeneo muliya-*point* moja moja na kamati itakuja kupewa, ili kwenda kuyangalia kwa kadri yalivyojitokeza kwenye *Hansard* ambayo Waheshimiwa Wajumbe mlichangia.

Eneo la pili ni maeneo ambayo yalikuwa yanatumiwa na wananchi kwa shughuli zao za kuendesha maisha, lakini yamechukuliwa bila ya kuzingatia maslahi ya wananchi waliokuwa wanayatumia. Vile vile yapo maeneo ambayo muliyataja kwamba wananchi walikuwa wananufaika kwa kuyatumia, lakini hatimaye yakawa yamechukuliwa ambapo hayakuzingatia maslahi ya wananchi.

Tatu wawekezaji wanaochimba mchanga kwenye maeneo ya fukwe. Waheshimiwa Wajumbe, kuna maeneo ya ardhi kwenye fukwe yanachimbwa mchanga na wawekezaji nayo yalitajwa na yataonekana kwenye *Hansard* kama mulivyoyaeleza, ili muweze kufuatilia na hatimaye ripoti italetwa hapa.

Nne mgogoro wa ardhi baina ya serikali na wananchi, yaani wakulima huko Bambi na hii ilikuwa *very specific*.

Tano mgogoro wa ardhi baina ya mfanyabiashara na wakulima Tumbe na hii ilikuwa *very specific*.

Sita mgogoro wa maeneo ya ardhi ya wananchi yaliyonyang'anywa na kufanywa Vitega Uchumi Makangale. Kwa hivyo, mtaangalia na hatimaye mtaviripotia na vipi wananchi hao walinyang'anywa na kama kuna mazingatio mengine mtakuja kuona hapo baadaye Kamati itakapofuatilia eneo la Makangale.

Saba mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na viongozi wa serikali Mchangamle Kizimkazi. Pia mtaangalia hiyo na mtaturipotia jambo gani la kuweza kufanywa katika hapo kama mtakavyoona inafaa Waheshimiwa Wajumbe ambao ni wanakamati teule na hatimaye Baraza.

Nane mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na Watendaji Wakuu wa Serikali Vitongoji Makaani nayo ilikuwa *very specific*, naomba mfuatilie huko.

Tisa mgogoro wa ardhi na wanakijiji na mwekezaji Pwanimchangani nayo ilikuwa ni *very specific*, mtaangalia na kutuletea hiyo taarifa.

Kumi mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na Viongozi Wakuu wa Juu wa Serikali Tondooni Mkunguni Pemba. Waheshimiwa Wajumbe, mimi wala sikujui lakini imetajwa hivyo na mtafuatilia na mtaturipotia na kutupendekezea nini kifanywe.

Kumi na moja mgogoro wa ardhi baina ya Idara ya Upimaji na Ramani na Wizara ya Kilimo Tumbe, mgogoro ambao umepelekea wananchi kulivamia eneo hilo, nalo mulilisema Waheshimiwa Wajumbe kwa hiyo lifuatiliwe, ili tuone nini cha kufanya.

Mwisho kumi na mbili mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na mwekezaji Shehia ya Mzwaridini Bwejuu na hii ilikuwa *very specific*. Jambo hili ni gumu kidogo Waheshimiwa Wajumbe, tunaombwa Kamati Teule ile ifanyekazi hiyo ambayo ni ngumu kwa mujibu wa maelekezo hayo ambayo Waheshimiwa Wajumbe mumeyatoa.

Kwa kweli ni kazi nzito kidogo na inabidi tufanyekazi kwa uadilifu, kwa umuhimu, ili tupate taarifa itakayoelekeza Baraza hili na hatimaye serikali nini cha kufanya juu ya migogoro hiyo, ili tufike pahala kwamba hiyo migogoro ipungue au kuondoka kabisa.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwasilisha kazi hiyo muliyonituma, ili shughuli zetu za Baraza na serikali ziwe zinakwenda kwa ufanisi mzuri tena wa kima kikubwa kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu pamoja na watu wake.

Matangazo mengine nadhani nitayatoa hapo baadaye kidogo baada ya kusikiliza Hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Kiongozi wa Shughuli za Serikali ndani ya Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba baada ya hayo nimkaribishe sana kwa heshima na taadhima Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, afya njema na kutujaalia amani na utulivu katika taifa letu. Naomba pia nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa busara zako za kuweza kuliendesha Baraza lako Tukufu kwa umakini na mafanikio makubwa.

Pia nawashukuru na kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa namna wanavyokusaidia Mhe. Spika katika kuliongoza Baraza hili. Vile vile, nawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali za kudumu kwa kazi zao nzuri wanazozifanya katika kufuatilia utekelezaji wa taasisi mbali mbali za serikali na kufanikisha mkutano huu.

Mhe. Spika, Mkutano huu wa Nane wa Baraza la nane umekuwa wa kihistoria katika nchi yetu kutokana na mashirikiano makubwa ya Viongozi na Wajumbe wa Baraza na Watendaji wa Taasisi za Serikali. Nawashukuru wote na naomba tuendelee na mashirikiano haya mazuri.

Mhe. Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake wa busara, hekima na unaozingatia maslahi ya wananchi. Ni dhahiri kuwa bidii za Rais Shein zinaendelea kuzaa matunda ya maendeleo katika sekta za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mhe. Spika, vile vile niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwasilisha bajeti zao vizuri na kuweza kujibu hoja mbali mbali zilizojitokeza kwa umahiri na uelewa mkubwa.

Mhe. Spika, napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wa Baraza lako Tukufu kwa kujadili, kudadisi na hatimae kupitisha bajeti za mapato na matumizi ya wizara zetu. Naelewa kwamba hoja zao mbali mbali walizoziibua zilikuwa na mwelekeo mzuri na nia njema ya kuisaidia Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hii imeonesha namna ambavyo Wajumbe wako walivyofahamu mafunzo mbali mbali uliyowapa. Hata wananchi wetu ambao wametutuma kuja kuwawakilisha wanafurahishwa na jinsi Wajumbe wanavyochangia na kuibua hoja mbali mbali za msingi zenye nia ya kuiletea tija nchi yetu.

Mhe. Spika, nampongeza kwa dhati rafiki yangu Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na namtakia mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yake ya kumsaidia Mhe. Rais katika kuiongoza sekta hii muhimu ya Miundombinu na Mawasiliano. *(Makofi)*

Pia nachukua nafasi hii kumpongeza aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Hamad Masoud Hamad ambae ni Mwakilishi wa Jimbo la Ole kwa ujasiri wake aliyouonesha wa kuwajibika kisiasa kufuatia ajali ya meli ya M.V Skagit. Yeye hakuhusika moja kwa moja na ajali hiyo, lakini ameona ni vyema kuwajibika kisiasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, natoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Marina Joel Thomas kwa kuteuliwa kwake kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nachukua fursa hii kumkaribisha Mhe. Marina katika kujumuika na Waheshimiwa Wajumbe wenzake katika kuchangia maendeleo ya taifa letu. Kuteuliwa kwake huko kunaonesha imani kubwa ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayo juu yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda pia nimshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Yahya Khamis Hamad pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao, juhudi ambazo zimepelekea kufanikiwa kwa mkutano huu wa Nane wa Baraza hili.

Aidha, napenda kumpongeza Katibu wetu wa zamani, Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim kwa kuteuliwa kwake na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Namtakia kila la kheri na mafanikio mema katika kazi yake hiyo mpya yenye changamoto nyingi.

Mhe. Spika, vile vile nachukua nafasi hii kuvishukuru vyombo vya habari vyote hasa Shirika la Habari la Zanzibar kupitia *Radio* na *TV* ambavyo vilirusha moja kwa moja maendeleo na shughuli za Baraza na kuwezesha wananchi wetu kufuatilia kwa makini hoja, michango na mijadala iliyokuwa ikiendelea Barazani hapa.

Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru wakalimani wa lugha ya alama kwa kazi zao nzuri walizozifanya kutafsiri mijadala kwa ishara ili wananchi wetu wenye ulemavu wa kutokusikia, nao waweze kufuatilia mijadala yetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niwashukuru wananchi kwa kuonesha shauku ya kufuatilia mijadala na michango mbali mbali iliyokuwa ikiendelea katika Baraza hili. Hii inaonesha jinsi wananchi walivyohamasika katika kuitumia haki yao ya kupata habari mbali mbali na taarifa za Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza hili la Bajeti kwa mwaka 2012/2013 limefanyika bila ya kuwa na wenzetu wawili Mhe. Mussa Khamis Silima (aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini) na Mhe. Salum Amour Mtondoo (aliyekuwa Mwakilishi wa Bububu) ambao wametangulia mbele ya haki. Tutaendelea kuwakumbuka kwa michango yao mikubwa waliyoitoa katika Baraza hili. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yao na kuziweka roho zao mahala pema peponi, Amin.

KUIMARIKA MFUMO WA SERIKALI YA UMOJA WA KITAIFA:

Mhe. Spika, hivi sasa inakaribia miaka miwili tangu kuwa na Serikali yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa. Ni jambo la faraja kuona nchi yetu inaendelea katika hali ya amani na utulivu. Nachukua tena fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake katika kuiongoza nchi yetu.

Pia nampongeza sana Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa jinsi anavyotekeleza majukumu yake vizuri ya kumshauri na kumsaidia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, shukurani za kipekee nazitoa kwa Viongozi wote wa Serikali, Vyama vya Siasa na wananchi kwa jumla kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa Serikali yetu. Waheshimiwa Wawakilishi wameonesha kuwa na upeo mkubwa wa majadiliano na udadisi katika utoaji wa hoja na michango yao ndani ya Baraza.

Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kujibu hoja na kutoa ufafanuzi wa kina katika masuala mbali mbali yaliyojadiliwa katika Baraza hili, jambo ambalo linadhihirisha kukua kwa demokrasia na kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji wa Baraza letu.

Kama ilivyosisitizwa ndani ya Baraza hili na Waheshimiwa Wajumbe, nami napenda kuwasisitiza Waheshimiwa Mawaziri kwamba wasikubali kuwekwa mikiani, lazima wasimamie vyema matumizi ya fedha za serikali zilizopitishwa na Baraza hili katika wizara zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ningependa kuelezea tatizo la utoro wa baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, na hata baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri ambapo wakati mwengine unalazimika kuakhirisha shughuli za Baraza kwa muda kama ilivyotokea tarehe 25 Julai, 2012 ili kungojea Wajumbe watimize akidi (*quorum*) kabla ya kuendelea na shughuli zake. Ninawasihi sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kuacha tabia hii, kwani wananchi waliotutuma kuwawakilisha hapa wanatuona na kutushangaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi mwenyewe nikiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Barazani, nawajibika pia kuwepo Barazani kwa muda wote Baraza linapoendelea. Lakini kwa nafasi yangu nikiwa Kiongozi wa Kitaifa wakati mwengine nalazimika kukosekana Barazani sio kwa sababu ya kupanga kwangu au kudharau shughuli za Baraza, bali ni kwa sababu ya kutekeleza majukumu mengine ya kitaifa ambayo yanahitaji mahudhurio yangu na wakati mwengine kutakiwa hata kumuwakilisha Mhe. Rais katika shughuli za Kitaifa ambazo asingeweza kuhudhuria yeye mwenyewe.

Hata hivyo, kukosekana kwangu Barazani Mhe. Spika anakuwa na taarifa zangu zote. Vile vile utaratibu upo wa Serikali kupata hoja za Wajumbe kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri. Ni vyema nikawakumbusha Waheshimiwa Wajumbe kwamba kama Kiongozi wa Kitaifa, mbali na jukumu hili la Baraza bado nakabiliwa na majukumu mengine ya kitaifa ambayo yanahitaji kushughulikiwa sambamba na jukumu hili la Baraza. Mambo yote hayo, yana nia ile ile ya kuwatumikia wananchi wetu.

MASUALA MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA BARAZA:

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa Nane wa Baraza lako Tukufu, Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zetu zote walipata fursa ya kuwasilisha na kupitishiwa bajeti zao za makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2012/2013 pamoja na kueleza programu mbali mbali watakazo zitekeleza kwa kipindi hichi. Aidha, katika mkutano huu Miswada miwili ya Sheria imewasilishwa ambayo ni:

1) Mswada wa Fedha (*Finance Bill*);

2) Mswada wa Matumizi (*Appropriation Bill*).

Aidha, katika mkutano huu Waheshimiwa Wajumbe wamepata fursa ya kushiriki katika semina tano muhimu zilizolenga kuwaongezea Wajumbe uzoefu na taaluma katika masuala yafuatayo:-

1. Semina kuhusu Mfumo wa Bajeti na Kanuni zinazoongoza Mijadala ya Bajeti.

2. Semina ya Kuwawezesha Wajumbe Wanawake katika Masuala ya Jinsia na Mawasiliano.

3. Semina ya Mashauriano baina ya Wenyeviti wa Kamati za Baraza na Maafisa Utafiti wa Baraza.

4. Semina ya Kupitia Ripoti za Wataalamu kuhusiana na "*Database*" ya Wadau wa Kamati ya Baraza na Uwezo wa Wajumbe katika utungaji Miswada.

5. Semina kuhusu Elimu ya Katiba kwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa ushiriki wao katika mijadala ya Miswada ya Sheria na katika mada za Semina zilizowasilishwa, na ni imani yangu kwamba Wajumbe wamepata uwelewa mzuri wa masuala yaliyowasilishwa na hivyo itawasaidia katika shughuli zao ndani ya Baraza. Nakupongeza Mhe. Spika, kwa juhudi uliyochukua mpaka kufanyika kwa Semina hizo.

MSIBA WA KUZAMA KWA MELI:

Mhe. Spika, mnamo tarehe 18 Julai, 2012 nchi yetu ilikumbwa na msiba mwengine mkubwa wa kuzama kwa meli ya M.V Skagit kwenye mkondo wa Kibaazi (meli saba kutoka kisiwa cha Chumbe). Meli hiyo iliyokuwa ikitokea Dar-es-Salaam kuja Zanzibar ilisadikiwa kuwa na abiria 290. Idadi hii ni kwa mujibu wa manifest iliyotolewa na wamiliki wa meli hiyo.

Katika ajali hiyo, jumla ya waliokolewa wakiwa hai ni watu 146 na hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2012 ni maiti 136 wamepatikana ambao maiti 75 wametambuliwa na jamaa zao na 61 hawakuweza kutambuliwa na hivyo mazishi yao yamesimamiwa na Serikali. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi, Amin. Kwa wale waliokolewa wakiwa hai tumuombe Mwenyezi Mungu awazidishie uzima na awape afya njema. Aidha, Mwenyezi Mungu awape uvumilivu na subira wale wote walioguswa na msiba huo kwa kupoteza ndugu na jamaa zao.

Mhe. Spika, serikali inawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwa njia moja ama nyengine katika operesheni za uokozi, mazishi na huduma nyengine zote zinazohusiana na maafa haya. Aidha, serikali inapenda kuwashukuru wale wote waliotoa michango yao ya hali na mali kwa ajili ya kuwafariji na kuwasaidia waathirika wa ajali hii.

Mhe. Spika, wakati wa msiba huu mzito Viongozi Wakuu wa nchi yetu walikuja kutufariji akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Ali Hassan Mwinyi, Waziri Mkuu wa Tanzania, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliyemaliza muda wake Mhe. Dkt. Asha Rose Migiro.

Mhe. Spika, vile vile nachukua fursa hii adhimu kutoa shukurani za Serikali kwa Waheshimiwa Mabalozi mbali mbali, Wakuu wa Makampuni na Mashirika mbali mbali kwa kutufariji na kwa misaada yao. Tunatoa shukurani nyingi kwa Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama ikiwemo Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Polisi, KMKM, Chuo cha Mafunzo na Kikosi cha Zima Moto na Uokozi kwa jitihada zao kubwa katika operesheni za uokozi.

Tunawashukuru pia vikundi vya wazamiaji wa kujitolea vya *Island Marine* ya Malindi, *Easy Blue Divers* ya Jambiani na Jumuiya ya Wavuvi wa Kojani (*KOFDO*) kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi chote cha uokozi. Aidha, tunawashukuru wenzetu wa *Red Cross*, Wizara ya Afya, Wamiliki wa Mahoteli, Wamiliki wa vyombo vya usafiri wa baharini, vijana wetu wa Skauti, Viongozi wa Dini, Kamisheni ya Wakfu, Ofisi ya Mufti na Wajumbe wote wa Kamati ya Taifa ya Kukabiliana na Maafa kwa mashirikiano yao makubwa katika kukabiliana na maafa haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali tayari imeshaunda Tume ya kuchunguza kuzama kwa meli ya M.V Skagit, ili kupata taarifa sahihi juu ya ajali ya meli hiyo. Tume hii ya watu kumi inaongozwa na Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar Mhe. Abdulhakim Ameir Issa.

UKIMWI:

Mhe. Spika, Ukimwi bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu. Hii ni kutokana na athari zake kiuchumi na kijamii. Ni vyema wananchi tukaelewa kwamba dunia bado haina tiba sahihi ya maradhi haya thakili. Hivyo ni wajibu wetu

wananchi sote kujizuia na vitendo vyote vinavyoweza kupelekea kupata maambukizi ya maradhi haya. Aidha, nawasihi wananchi kuacha tabia ya kuwanyanyapaa wale wenzetu ambao kwa bahati mbaya tayari wameshapata maambukizi. Ni vyema kila mmoja wetu kuchukua hatua ya kuchunguza afya yake ili kujua kama yuko salama au amepata maambukizi ili kuchukua hatua za mapema zinazostahiki kwa ajili ya kuimarisha afya yako.

MWEZI MTUKUFU WA RAMADHAN

Mhe. Spika, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kutekeleza ibada ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Tumuombe Mwenyezi Mungu atutakabalie funga na ibada zetu na atujaalie tumalize Ramadhani kwa salama na amani, Amin.

Mhe. Spika, tukimaliza mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunakabiliwa na Sikukuu adhimu ya Idd el Fitri. Kwa vile hatutaweza kukutana hapa katika hali hii, napenda kuchukua fursa hii, kutoa mkono wa Idd Mubarak kwa Wajumbe wote na kuwatakia Sikukuu njema wananchi wote na kuwataka kufurahia sikukuu hiyo kwa furaha, utulivu na amani. Nawaomba madereva wa vyombo vya moto na watumiaji wengine wa barabara kuwa waangalifu wakati wanapotembea barabarani ili kuepuka ajali zisizo za lazima.

HITIMISHO:

Mhe. Spika, nazidi kuwaomba wananchi waendelee kuishi kwa amani, umoja na upendo na kuacha vitendo vyovyote vya uvunjifu wa sheria na vitakavyo ashiria uvunjifu wa amani na utulivu. Rasilimali kubwa ya Wazanzibari ni amani na utulivu. Naomba kila mmoja wetu atimize wajibu wa kulinda amani na utulivu uliopo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia, naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza na Baraza lako Tukufu pamoja na wananchi. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako pamoja na wananchi wote kwa kunisikiliza. Vile vile, napenda kuwatakia Wajumbe wote wa Baraza hili safari njema ya kurudi Majimboni mwao kwenda kuwatumikia wapiga kura wao.

Mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wake zangu, Bibi Pili Juma Iddi na Bibi Asha Suleiman Mohammed kwa kunisaidia na kunivumilia wakati wa kipindi chote cha Baraza. Shukrani za pekee ziende kwa Bi. Asha kwa kusimamia vyema shughuli za Jimbo langu la Kitope wakati nikiwa katika shughuli za Baraza.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako Tukufu hadi siku ya Jumatano, tarehe 10 Oktoba, 2012 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Saa 5:38 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 10/10/2012 saa 3.00 asubuhi)